

# Dai Pesa Zako



Huenda unastahili kupata hadi **\$6,000** au zaidi katika rudisho yako ya ushuru unapodai **Rudisho ya Ushuru wa Kazi (Earned Income Tax Credit)** na **Rudisho ya Ushuru kwa Watoto (Child Tax Credit)**

1

## Pata sehemu ya BURE ya ushuru\*

Tazama [irs.treasury.gov/freetaxprep](https://irs.treasury.gov/freetaxprep) au piga simu **800-906-9887**.

2

## Angalia kama unastahili

Tambymuch unaweza kupokea katika [eitcoutreach.org/help](https://eitcoutreach.org/help).

3

## Jaza fomu zako za ushuru

Tembelea tovuti ya bure kabla ya Aprili 15 ili uandikishe ushuru yako na kupokea pesa yako kwa kurudishiwa ushuru.

\*Bado unaweza kudai rudisho za ushuru (tax credits) hata kama huwezi kupata mahali pa ushuru bila malipo karibu yako.

### ***Lini utajaza fomu zako za ushuru?***

Tarehe:

Saa:

Mahali:

Simu:

Kwa maelezo zaidi, tazama [eitcoutreach.org/help](https://eitcoutreach.org/help) au pigia simu IRS kwa **1-800-829-1040**.

GET IT  
BACK

SW

# JE, NASTAHILI?

Rudisho ya Ushuru wa Kazi (Earned Income Tax Credit) na Rudisho ya Ushuru kwa Watoto (Child Tax Credit) ni mafao ya ushuru kwa watu wanaofanya kazi. Huenda utadaiwa ushuru wa chini zaidi na urudishiwe pesa taslimu!

Kudai rudisho hizi hakutaathiri kustahili kwako kwa mafao kama SNAP (stampu za chakula), SSI, Medicaid, usaidizi wa fedha, au nyumba za jamii. Rudisho zinazowekwa akaunti ya akiba hazihesabiwi dhidi ya viwango vya programu/taasisi za usaidizi zinazodhaminiwa na serikali miezi 12 baada ya rudisho kupokewa.

## KAMA UNA WATOTO

- Umri:** Kwa EITC, watoto lazima wawe na umri usiozidi miaka 19 mwisho wa 2019 (wanaosoma muhula mzima wanaweza wasizidi miaka 24 na watoto wenye kilema kiasi au kamili wanaweza kuwa wa umri wowote). Kwa CTC, watoto lazima wawe na umri usiozidi miaka 17 mwisho wa 2019.
- Makao:** Watoto lazima wawe wameishi nawe kwa zaidi ya nusu ya 2019.
- Mapato ya 2019:** Kwa CTC, kama ulipokea zaidi ya \$2,500, unaweza kudai hadi \$2,000 kwa kila mtoto.

Kwa EITC, mapato yako lazima yawe chini ya viwango vifwatavyo:

Watoto	Haujafunga ndoa	Umefunga ndoa	EITC hadi:
1	\$41,094	\$46,884	\$3,526
2	\$46,703	\$52,493	\$5,828
3 au zaidi	\$50,162	\$55,952	\$6,557

### Nini unastahili kuleta katika mahali pa ushuru bila malipo

- Kitambulisho halali chenye picha
- Kadi ya Hazina ya Jamii (Social Security Number), barua ya thibitisho la kuwa na Social Security Number, au ITIN
- Fomu za W-2 au 1099
- Fomu ya 1095-A

## KAMA HAUNA WATOTO

- Umri:** Lazima uwe na umri wa kati ya miaka 25 na 64.
- Mapato ya 2019:** Kama ulipokea mapato yasiyozidi \$15,570 (\$21,370 kama umeowa/umeolewa), unaweza kurudishiwa hela za EITC hadi \$529.

## KAMA WEWE SI MWANANCHI

- EITC:** Wewe, mume/mke wako, na mtoto yeyote unaemshughulikia lazima muwe na Namba halali ya Hazina ya Jamii (Social Security Number).
- CTC:** Wewe na mume/mke wako lazima muwe na Nambari ya Huduma za Malipo ya Kijamii (Social Security Number) au Nambari ya Utambulisho wa Binafsi ya Kodi (Individual Taxpayer Identification Number, ITIN). Mtoto yeyote unayemdai lazima awe na Nambari ya Huduma za Malipo ya Kijamii (Social Security Number).

### Bima ya Afya

Unaweza kustahili bima ya afya ya bure au ya gharama nafuu katika Medicaid au kwa Kodi wa Mikopo ya Bima. Jiunge na Medicaid wakati wowote au katika HealthCare.gov kati ya Novemba 1, 2019 na Dec.15, 2019. Pata maelezo zaidi kwa **1-800-318-2596** au **www.HealthCare.gov**.